OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA

Addresss "LONDONI", SONGEA
Direct line: 0757 673758
Mob: 0763823516

SHULE YA SEKONDARI LONDONI,
S. L. P 621,
SONGEA
30/03/2022

Kumb. na Lond SS/JI/VOL.1/ 04

Mzazi/Mlezi wa……...

S.L.P……

…….

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LONDONI KIDATO CHA TANO 2022/2023

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **2022/2023**.Shule ya sekondari Londoni iko kata ya Lizaboni, umbali wa kilometa tano kutoka kituo cha mabasi zamani, kusini magharibi mwa manispaa ya Songea**, b**arabara ya kuelekea Peramiho. Aidha,mwanafunzi anatakiwa kusafiri na fomu yake ya kujiunga na ataionesha kwa mhudumu wa basi husika mwisho wa safari ili kupata msaada zaidi wa namna ya kufika shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe**…….** Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …….

1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.1 SARE YA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote wa masomo, anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa kwenye shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule. Aidha, lipo vazi la kazi za nje ambalo huvaliwa na mwanafunzi anapokuwa katika kazi za mikoni baada ya masomo.

(a) Shati nyeupe (blauzi mbili au zaidi za mikono mifupina mikono mirefu kwa waislamu).

(b) Sketi mbili (2) rangi ya kahawia pamoja na Tai ya kahawia yenye alama "V nyeupe".
TANBIHI: ILI KUEPUSHA UTOFAUTI WA RANGI YA KITAMBAA CHA SKETI, MWANAFUNZI AJE ASHONE HUKU SONGEA, GHARAMA YAKE NI SH.30,000/= KWA KILA SKETI MOJA.

(c) Raba nyeupe za kamba zisizo na mchanganyiko wa rangi, zisiwe na visigino virefu (High heels) jozi 2.

(d) Sweta moja au zaidi la kuvaa wakati wa baridi, la kahawia sawa na rangi ya sketi, lisiwe la kufumwa.

(e) Soksi nyeupe ndefu mbili au zaidi.

(f) Hijabu nyeupe kwa waislamu.

1.2 VAZI LA KAZI

Gauni la kazi la rangi ya light blue (Esteem no 1), Ili kuepusha utofauti wa rangi na namna ya ushonaji, mwanafunzi aje ashone huku ,gharama yake ni shilingi 28,0000/=). Waislamu waje na hijabu nyeupe.

1.3 SARE YA MICHEZO

(i) Track suit nyeusi (**adidas**) yenye mistari ya rangi nyeupe isiwe na kofia.
(ii) T-shirt yenye kola na nembo ya shule 1 (zinapatikana shuleni kwa gharama ya sh.12,000/=).
(iii) Bukta pamoja na fulana nyekundu 1 na bluu 1.
(iv) Raba nyeusi za kamba.

1.4 MAVAZI YA MSIKITINI (KWA WAISLAMU)

(i) Suruali nyeusi na pana
(ii) Blauzi nyeupe ndefu na pana yenye mikono mirefu (nusu kanzu)
(iii) Hijabu nyeupe

NB: KAMWE MWANAFUNZI ASIJE NA NGUO NYINGINE ZISIZOELEKEZWA.

2. ADA NA MICHANGO YA SHULE

2.1 ADA YA SHULE

Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs. 70,000/=. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula.Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Na. **61801200163** katika benki ya **NMB**. Jina la akaunti ni **Londoni Secondary School** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

2.2 MICHANGO MINGINE

(i) Ukarabati TShs. 15,000/= kwa mwaka
(ii) Kitambulisho na picha TShs. 6,000/=
(iii) Taaluma TShs. 20,000/= kwa mwaka
(iv) Wapishi, walinzi na vibarua wengine TShs. 30,000/= kwa mwaka
(v) Tahadhari ni Tshs. 5,000 (mara moja tu na haitarejeshwa)
(vi) Mitihani ya kujipima Tsh. 20,000/=
(vii) Afya 15,000/= (Huduma ya kwanza).
(viii) Mzazi mkatie mwanao Bima ya afya ya NHIF (kwa wale wasiokuwa nazo,mwnwfunzi aje na pesa taslimu sh. 50,400/= ili shule imunganishe,**na huu si sehemu ya mchango wa shule**.

Fedha hizo **zilizo ainishwa kipengele Na. 2.2** zilipwe kwenye akaunti ya shule Na.**61801200163**, isipokuwa fedha ya mtihani wa kujipima na fedha ya bima ya afya kwa wale wasiokuwa nazo zilpwe kwenye akaunti Na **61806600005** katika benki ya **NMB**. Jina la akaunti ni **Londoni Secondary School** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

3. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

(i) Ndoo mpya mbili (kubwa 1,ndogo 1).
(ii) Ream 2 za karatasi (A4) kwa mwaka.
(iii) Mfagio wa nje (chelewa) 1,
(iv) Drier squeezer 1
(v) Mfagio laini wa ndani 1 (soft broom)
(vi) Brashi ngumu yenye mshikio mrefu 1. (Hard broom)
(vii) Brashi ndogo ya kusafishia masinki ya choo 1
(viii) Jembe moja lililonolewa na mpini wake.
(ix) Kwanja (slasher) moja lililonolewa.

4. MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI

(i) Sanduku linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake (Trunker).
(ii) Godoro la ft 2½ upana.
(iii) Chandarua.
(iv) Mto na foronya yake rangi nyeupe au light blue.
(v) Blanketi 1.
(vi) Bed cover 2 rangi ya light blue.
(vii) Shuka za kulalia 2
(viii) Taulo 1
(ix) Mwamvuli 1
(x) Vitenge/Khanga pair moja.
(xi) Kandambili umoja nyekundu
(xii) Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe na kijiko
(xiii) Daftari zaidi ya ishirini (Counter Books)
(xiv) Mathematical set 1(kwa wanaosoma EGM, HGL na HGK)
(xv) Scientific Calculators (isiyo programmable) fx-991MS (kwa wanaosoma EGM, HGL na HGK)
(xvii) Graph pad 1 (kwa wanaosoma EGM, HGL na HGK) isipokuwa wenye tahasusi ya HKL.
(xviii) Vitabu mbalimbali kulingana na masomo anayosoma:

A. HISABATI

i. **Understanding Mathematics**
ii. **Conceptual Advanced Mathematics-volume I&II –PL M**
iii. **Pure Mathematics volume I &II**
iv. **Understandable Advanced Mathematics-volume I&II**
v. **Non-programmable calculator fx.991 MS OR fx.991 ES**

B. ENGLISH LANGUAGE

i. **Advanced Oxford Dictionary (ni lazima)**
ii. **Comrehensive Linguistics form 5&6-Mgonja .**M, E

iii. **Advanced English Language 01-**Nicholaus Ashel

iv. Contemporary English for Advanced form 5&6

v. Advanced Level Literature-Nicholaus Ashel

vi. Readings:

- **PLAYS.**
  Betrayal in the City-Francis Ibuga
  An Enemy of the People-Henrich Ibsen
  Iwill Marry when Iwant-Ngugi Wa Thiongo
  Lwanda Magere=Okoiti Omtah
  The Bride-Austine Bukenya
  The Black Mamba-John Ruganda

- **NOVELS**
  Beautyful ones are Not Yet Born-Ayi Kwei Ammar
  A Man of the People-Chinua Achebe
  Encounter from Africa-Macmillan Ed. LTD
  The season of Waiting-David Onowale
  The Devine Providence-Severine N. Ndunguru
  Vanishing Shadows –Namige Kayombo

- **POETRY**
  Selected Poems-Institute of Education
  Wonderful Surgeon and other poems- Charles Mlokwa

C. KISWAHILI

- **TAMTHILIYA**
  Nguzo Mama-Penina Mhando
  Kivuli Kinaishi-Said A, Mohamed
  Morani-Emmanuel Mbogo
  Kwenye Ukingo wa Thim-Ebrahim Hussein

- **RIWAYA**
  Vuta n'Kuvute-*Shafi Adam Shafi*
  Mfadhili -Hussein Tuwa
  Kufikirika-Shaban Roberts
  Usiku Utakapokwisha-Mbunda Msokile

- **USHAIRI**
  CHUNGU Tamu-Theobald Mvungi
  Fungate ya Uhuru-Mohamed s. Khatibu
  Kimbunga-Haji Gora
  Mapenzi Bora-Shaban Roberts

D. GEOGRAPHY

1. **Research Methodology** –C, R Kothari
2. **Landforms in Africa:An introduction to Geomorphology**-Coln Buckle
3. **General Geography in Dragrams**-R. B Bunnett
4. **Practical Geography** –John, M. Pritchard
5. **Physical Geography Alive**-Zisti Kamili
6. **Physical Geography for Secondsry Schools**-D. T Msabila
7. **Human and Economic Geography=Zisti Kamili**

E. ECONOMICS

1. **Macroeconomics For Advanced Secondary Schools.Student Book Form Five and Six-**Tanzania Institute of Education
2. **Microeconomics For Advanced Secondary School.Student Book –**Tanzania Institute of Education
3. **Economics made Simple paper one (Second edition)-**E.B Mwakagile
4. **Economics Made Simple paper two=E.**B MWAKAGILE
5. **Advanced Level and Professional Studies, economics paper one/paper two-**Ambilikile

F. HISTORY

1. **History paper 1&2 lesson notes for Advanced certificates of secondary Ed. Bakari Madaya.**
2. **Fundamental principlesof History. MAGOTI BERNARD (Paper 1&2)**
3. **Essential History for Advanced History. (paper 1 & 2)**

5. FEDHA ZA MATUMIZI KWA MWANAFUNZI

Mzazi unashauriwa umpe fedha za kutosha kwa matumizi yake, kuna duka la shule ambalo huwauzia wanafunzi mahitaji yao. Aidha, hairuhusiwi kuweka fedha nyingi bwenini. Hivyo anatakiwa kufungua akaunti Benki ya Posta, NMB, NBC au CRDB zilizopo hapa Songea kwa ajili ya kutunzia fedha zake.**Pia fedha za matumizi zinatakiwa zitumwe kupitia simu ya shule namba 0679899336 kisha andika ujumbe kiasi ulichotuma na jina la mwanafunzi husika. Namba zote zimesajiliwa kwa jina la shule.**

6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

A. HESHIMA

1. Mwanafunzi asimame na kumsalimia Mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mkutano.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yake na wenzake, kwa mwalimu wake na kwa watu wengine.
3. Mwanafunzi awaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
4. Mwanafunzi ashirikiane na kusaidiana na wenzake katika kazi.
5. Mwanafunzi athamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:- (a) Kuvuta sigara.
   (b) Kufuga kucha ndefu.
   (c) Kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
   (d) Kufuga ndevu.
   (e) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
   (f) Kugombana.
   (g) Kumiliki au kutumia simu ya mkononi au kifaa chochote kinachohusiana na simu ya mkononi.**MAWASILIANO YOTE YATAFANYIKA KUPITIA OFISI YA MALEZI.**
7. Mwanafunzi aitike mara moja na kukimbilia anakoitwa.
8. Mwanafunzi aheshimu Bendera ya Taifa (Serikali), picha za viongozi wa wakuu wa Serikali, Nembo ya Taifa (Coat of Arms), Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
9. Mwanafunzi aheshimu na kutunza ukumbi wa mikutano, mahali pa kuliachakula, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.
10. Mwanafunzi anatakiwa kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
11. Mwanafunzi awe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote alipo.
12. Mwanafunzi anyooshe mkono juu na kusimama anapoulizwa na kujibu maswali.

Mwanafunzi akae kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ya ruhusa ya mwalim au kiongozi aliyeko.

NB: SIMU ZA MKONONI HAZIRUHUSIWI KABISA HAPA SHULENI. MWANAFUNZI ASIRUHUSIWE KUJA NA SIMU. ADHABU KALI IKIWA NI PAMOJA NA KUFUKUZWA SHULE ITACHUKULIWA KWA ATAKAYEPATIKANA NA SIMU.

B. MAHUDHURIO

1. Mwanafunzi ahudhurie shule kwa muda wote wa masomo.
2. Mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa ikiwa ni pamoja na kuhudhuria maandalio ya masomo (preparation).
3. Mwanafunzi ahudhurie katika kazi zote za mikono.
4. Mwanafunzi ahudhurie mikutano ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano mingine.

C. KUWAHI

1. Kuwahi kuripoti mara shule inapofunguliwa.
2. Mwanafunzi awahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
3. Mwanafunzi atii mlio wa kengele na kuwahi anapohitajika.

D. MAWASILIANO

Mwanafunzi anapaswa kutumia lugha ya kiingereza wakati wote awapo shuleni, isipokuwa wakati wa somo la Kiswahili, au anapowasiliana na wafanyakazi wasio walimu pamoja na wageni.

E. SARE ZA SHULE

1. Kila mwanafunzi atavaa sare ya shule:
   (a) Wakati wote wa masomo ya darasani.
   (b) Wakati wote wa mihadhara ya shule (Baraza).
   (c) Wakati wa kwenda hospitalini/ mjini/ kwenye ibada/maandamano.
   (d) Wakati wote anapokuwa katika shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule.

1.5 SARE YA SHULE ISIVALIWE PAMOJA NA VITU VIFUATAVYO: -

- Kofia;
- Hereni; Bangili; pete;mikufu
- Viatu vya ghorofa
- Vibanio vya nywele
- Saa zenye marembo marembo (iwe na mkanda wa kawaida wa chuma, ngozi au plastiki).
- Kupaka rangi ya mdomo na ya kucha.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa viatu vya wazi jikoni.

F. MIPAKA YA SHULE

1. Mwanafunzi akisharipoti haruhusiwi wakati wa kuwa nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum.
2. Mwanafunzi atatembelea sehemu zifuatazo kwa kibali maalumu
3. (a) Jikoni.
   (b) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-
   (a) Vilabu vya pombe.
   (b) Majumba ya starehe.
   (c) Majumba ya kufikia wageni.

G. USAFI

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi na ni sehemu muhimu ya maisha yake ya kila siku. Kwahiyo kila mwanafunzi atazingatia yafuatayo:- (a) Usafi wa mwili wake na nguo zake.

(b) Usafi wa ukumbi wa chakula.

(c) Vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu.

(d) Usafi wa vyoo, madarasa, maabara, viwanja na barabara.

(e) Awe na nywele fupi – **njiti ya kiberiti ikichomekwa kwenye nywele ionekane. Haruhusiwi kusuka nywele.**

H. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi wa vitu na wizi wa kalamu (forgery).
2. Uasherati na uhusiano wa jinsia moja.
3. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji wa sigara na bangi.
5. Makosa ya Jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudu mali ya umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa na Nembo zingine za Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Ujauzito
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongeza vurugu au kuvuruga amani.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kulala nje ya bweni bila ruhusa.(utoro)
15. Kumiliki silaha ya aina yoyote.
16. Kumiliki kipasha joto (heater), pasi ya umeme, Radio, TV, Camera.
17. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule na kifaa chochote kinacho husiana na simu.
18. Kuto hudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
19. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
20. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
21. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi.
22. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
23. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kuua, au kutishia kujiua kwa sumu, n.k.

6. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

Pamoja na barua hii pokea:

A. Fomu Namba B ya kupimwa afya yake. Apimwe kwenye hospitali ya serikali, hakikisha anapimwa siyo kujaziwa fomu tu. Na umweleze mganga matatizo ya afya aliyonayo. Kwani hatutapokea hoja zozote kinyume na ripoti ya daktari.

B. Fomu Namba C ya kuonyesha ndugu wa karibu na ahadi ya utekelezaji wa wajibu.

C. Fomu Namba D ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

D. Uje na nakala za cheti cha kuzaliwa/affidavit certificate, Leaving certificate na result slip.

E. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi walioorodheshwa kwenye Fomu namba C.

NB: Uje na faili ndani ukiwa umeweka fomu Na. B, C, D na Viambatisho vilivyotajwa kwenye D na E hapo juu.

❖ **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA SAFARI NJEMA KUJA KUJIUNGA NASI.
KAULI MBIU (MOTTO WA SHULE) NI: "ELIMU BORA KWA MAISHA BORA"

KARIBU SANA LONDONI SEKONDARI

_____

ESTER E, KULUMULA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI LONDONI
S.L.P 621 SONGEA

KIAMBATISHO "B" PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

LONDONI SECONDARY SCHOOL,
P. O. B02OX 621, SONGEA.

_____

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine Miss _____ as to her physical and mental fitness for admission as a form FIVE at Londoni Secondary School for the Academic year 2020/2021Yours Sincerely,

……
ESTER E. KULUMULA
THE HEADMISTRESS

The Headmaster, I have examined Miss _____ as shown below and consider that she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full – time secondary school education.

1. Vision with/without glasses. Right _____
   Left_____
2. Blood pressure _____
   Hemoglobin _____
3. Hearing _____ 4. (a) Urine
   Albumen _____
   (b) Sugar_____ 5. (a) Venereal disease _____
   (b) Bilharzias _____
6. Pregnancy _____
7. Neurosis_____
8. Is there any abnormality of:
   (a) The heart _____ (b) Lungs_____
   (c) The spleen _____
9. Are there any serious disease e.g. leprosy, asthma, diabetes, etc
   _____
   Date_____
   Station _____ _____
   Signature of medical officer
   Designation _____

KIAMBATISHO 'C' Ndugu wa karibu: Hakikisha unaandika majina na anwani zao. Hii inaisaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo linatokea. Hatutaki majina ya ndugu wa bandia.

1. (a) Jina..... (b)Uhusiano .....
(c) Anuani:.....
(d) Kata:..... (e) Mtaa..... (f) Namba ya simu ..... (g)Balozi.....

2. (a) Jina..... (b)Uhusiano .....
(c) Anuani:.....
(d) Kata:..... (e) Mtaa..... (f) Namba ya simu ..... (g)Balozi.....

3. (a) Jina..... (b)Uhusiano .....
(c) Anuani:.....
(d) Kata:..... (e) Mtaa..... (f) Namba ya simu ..... (g)Balozi.....

4. (a) Jina.....(b)Uhusiano .....
(c) Anuani:.....
(d) Kata:..... (e) Mtaa.....
(f) Namba ya simu .....
(g)Balozi.....

Sahihi ya mzazi.....
Tarehe.....

AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU

 Mimi ..... nakubali nafasi niliyopata katika shule ya sekondari ya Londoni kuendelea na masomo.

 Nafahamu kuwa ninagharamiwa na Taifa linalothamini kazi na juhudi.

 Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema.

 Ninaahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha mwanafunzi kuachishwa shule.

 Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu/walezipamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule yangu na Taifa kwa ujumla.

.....
Sahihi ya Mwanafunzi

Mimi.....

Mzazi/mlezi wa ..... nimesoma maelekezo yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua. Ripoti na barua zote zinazohusu mtoto wangu ziletwe kwangu kwa anuani hiyo hapo chini:-

S. L. P .....
.....
……
Jina la mzazi..... Namba ya simu.....
Mtaa..... Balozi.....
Sahihi ya mzazi..... Tarehe.....

KIAMBATISHO 'D' FOMU YA MKATABA A. KATI YA MWANAFUNZI NA SHULE

1. Jina kamili kama alivyoandikishwa kwenye mtihani .....
2. Tarehe ya kuzaliwa.....
3. Mahali alipozaliwa.....
4. Dini..... Dhehebu.....
5. Shule alipomaliza elimu ya msingi..... Wilaya.....
   Mkoa..... Mwaka aliomaliza.....
6. Shule alipomaliza elimu ya sekondari (kidato cha nne).....
   Wilaya..... Mkoa..... Mwaka.....

Mimi..... ninaahidi kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai kama yalivyoainishwa katika sheria za shule na za nchi kwa ujumla.
Sahihi.....Tarehe.....

B. KATI YA MZAZI NA SHULE

Mimi..... Mzazi/Mlezi wa.....

Ninakiri na kukubaliana na sheria za shule kama ambavyo zimeainishwa kuwa mwanangu hatashiriki mgomo, fujo na makosa mengine ya jinai.
Aidha, nitakubaliana na hatua za kisheria atakazochukuliwa
mwanangu.....endapo atakiuka taratibu za shule.
Sahihi.....Tarehe.....